**FAHAMU HAKI ZAKO:**
**JAMBO LA KUFANYA UKISIMAMISHWA NA POLISI, AFISA WA UHAMIAJI AU AFISA WA FBI**
**Bila kujali hali yako ya uhamiaji au uraia, una haki za kikatiba!**

**UNA HAKI YA...**

- KUTOFUNGUA MLANGO WAKO isipokuwa wakati afisa wa ICE anapokuwa na hati ya idhini ya kukamata iliyotiwa sahihi na hakimu.
- KUTOJIBU MASWALI kuhusu hali yako ya uhamiaji au nchi unayotoka, wakati polisi, maafisa wa uhamiaji au maafisa wengine wowote wanapouliza.
- KUSALIA KIMYA NA KUKATAA KUIDHINISHA KUPEKULIWA KWAKO, gari lako au nyumba yako. Kusema “Ningependa kusalia kimya” na “Siidhinishi upekuzi wowote” kwa sauti ya juu ili maafisa na mashahidi wowote wakusikie.
- KUOMBA ULETEWE WAKILI ikiwa umekamatwa — usijibu maswali hadi mWAKILI wako awepo. Unaweza kukataa kutia sahihi kwenye hati bila kushauriana na wakili.
- KUULIZA "NIMEKAMATWA?” Ikiwa hujakamatwa, una haki ya kuondoka kwa utulivu.
- KUPOKEA HATI KATIKA LUGHA UNAYOELEWA. Ikiwa huelewi lugha ya Kiingereza, omba huduma za mkalimani.

**WAJIBU WAKO**

- Kuwa mtulivu na mwenye adabu.
- Beba kadi ya kijani, ikiwa unayo. Huenda ukalazimika kuwaonyesha maafisa wa uhamiaji. Ikiwa huna stakabadhi za uhamiaji, sema “Ningependa kusalia kimya.”
- Omba mkalimani ikiwa unamhitaji.
- Kumbuka maelezo ya kile kilichotokea.
- Usiwazuie polisi au maafisa wa uhamiaji kukukamata kwa kupigana nao.
- Usitoe taarifa za uongo, jina lisilo la kweli au hati bandia.

**JIANDAE KWA TUKIO LA KUKAMATWA NA ICE**

- Beba hii nawe ili ujue haki zako.
- Kumbuka nambari moja au mbili za simu za watu unaoweza kuwapigia simu ikiwa utakamatwa. Hutaweza kutumia simu yako baada ya kukamatwa.
- Hifadhi nakala za hati zako muhimu mahali salama ambapo mtu anaweza kuzipata, pamoja na dawa yoyote unayohitaji.
- Unda mpango wa dharura wa familia utakaotumika kuwatunza watoto wako ikiwa utakamatwa.

**UKISIMAMISHWA KWA AJILI YA KUHOJIWA**

- Kuwa mtulivu. Usikimbie. Usibishane au kuwazuia polisi, hata ikiwa huna hatia au polisi wanakiuka haki zako. Weka mikono yako mahali ambapo polisi wanaweza kuiona.
- Huhitajiki kujibu maswali yoyote, ikiwemo kutoa maelezo ya jina lako na nchi unayotoka. Unaweza kusema "Ningependa kusalia kimya."
- Uliza "nimekamatwa?” Ikiwa sivyo, ondoka kwa utulivu.

IKIWA UMESIMAMISHWA NA POLISI

- Maafisa wa polisi hawaruhusiwi kupekua (au kuomba kupekua) watembea kwa miguu na watoto isipokuwa maafisa wana sababu nzuri ya kuamini kuwa watu hao wanahusika katika uhalifu.
- Huhitajiki kukubali kupekuliwa au mali yako kupekuliwa. Polisi wanaweza "kupekua kuanzia juu hadi ya chini" mavazi yako ikiwa wanadhani una silaha.
- Ikiwa umekamatwa na polisi, una haki ya kujua sababu ya kukamatwa.

IKIWA UTASIMAMISHWA NA MAAFISA WA UHAMIAJI (“ICE”)

- Kumbuka: Huhitajiki kuzungumza. Maafisa wa ICE mara nyingi humkamata mtu baada ya kumuuliza jina tu.
- Usiwaonyeshe maafisa wa ICE kitambulisho kutoka nchi nyingine au utoe taarifa za uongo kuhusu uraia wako.
- Ikiwa maafisa wa ICE watasema kuwa wanakukamata, usijibu maswali yoyote. Salia kimya na uombe uletewe wakili. Unaweza kukataa kutia sahihi kwenye hati hadi pale utakapozungumza na wakili.
- Sema “Siidhinishi upekuzi wowote” ikiwa watapekua mifuko yako au mali yako.
- Maafisa wa ICE wanaweza kuwa na mashine za kutambua alama za vidole. Unaweza kukataa kuchukuliwa alama za vidole ikiwa hujakamatwa.

**UKISIMAMISHWA UKIWA NDANI YA GARI LAKO**

Simamisha gari mahali salama haraka iwezekanavyo. Zima gari, washa taa ya ndani, fungua sehemu ya kioo cha dirisha na uweke mikono yako kwenye usukani.

IKIWA UMESIMAMISHWA NA POLISI

- Wakiuliza, onyesha polisi leseni yako ya udereva, stakabadhi za usajili na uthibitisho wa bima.
- Ikiwa afisa ataomba kuangalia ndani ya gari lako, hupaswi kukubaliana na upekuzi huo. Ikiwa polisi wanadhani kuwa gari lako lina ushahidi wa uhalifu, gari lako linaweza kupekuliwa bila idhini yako.
- Madereva na abiria wote wana haki ya kusalia kimya. Ikiwa wewe ni abiria, unaweza kuuliza ikiwa uko huru kuondoka. Ikiwa afisa atasema ndiyo, keti kwenye gari na unyamaze au uondoke kwa utulivu. Kama abiria, huhitajiki kubeba kitambulisho, lakini unaweza kuombwa kukionyesha kwa afisa au kushiriki jina na anwani yako.

IKIWA UTASIMAMISHWA NA MAAFISA WA UHAMIAJI (“ICE”)

- Maafisa wa ICE wanaweza kuvalia fulana iliyoandikwa "Police" na wanaweza wasikwambie kuwa wao ni maafisa wa ICE. Waombe maafisa wakuonyeshe beji zao ili ujue shirika wanalofanyia kazi.
- Ikiwa maafisa wa ICE watasimamisha gari lako, huhitajiki kuonyesha kitambulisho chochote au kujibu maswali yoyote. Huhitajiki kuwaambia jina lako au kuwaambia nchi unayotoka. Sema “Ningependa kusalia kimya.”
- Ikiwa afisa wa uhamiaji ataomba kuangalia ndani ya gari lako, huhitajiki kukubali kufanyika kwa upekuzi huo. Sema “Siidhinishi upekuzi huu.”
- Una haki ya kuwa na wakili ikiwa utakamatwa — usijibu maswali yoyote ikiwa wakili wako hayupo.

**IKIWA POLISI AU MAAFISA WA UHAMIAJI WATAKUJA NYUMBANI KWAKO**

- Ikiwa polisi au maafisa wa uhamiaji watakuja nyumbani kwako, huhitajiki kufungua mlango isipokuwa wawe na hati ya idhini iliyotiwa sahihi na hakimu.

<u>IKIWA POLISI WATAKUJA NYUMBANI KWAKO</u>

- Waombe wapitishe hati ya idhini chini ya mlango au waishikilie kwenye dirisha ili uweze kuitazama.
- Hati ya idhini ya upekuzi inawaruhusu polisi kuingia kwenye anwani iliyoorodheshwa kwenye hati ya idhini, lakini maafisa wanaweza tu kupekua maeneo, na kwa vitu vilivyoorodheshwa.
- Hati ya idhini ya kukamatwa inawaruhusu polisi kuingia nyumbani kwa mtu aliyeorodheshwa kwenye hati hiyo ya idhini ikiwa wanaamini kuwa mtu huyo yuko ndani.
- Hata kama maafisa wa polisi wana hati ya idhini ya kukukamata kwa kosa la uhalifu, huhitajiki kuzungumza. Ukichagua kuzungumza na maafisa wa polisi, toka nje na ufunge mlango.

<u>IKIWA MAAFISA WA UHAMIAJI ("ICE") WATAKUJA NYUMBANI KWAKO</u>

- Maafisa wa uhamiaji hawawezi kuingia nyumbani kwako bila hati ya idhini iliyotiwa sahihi na hakimu. Hati zilizotiwa sahihi na maafisa wa ICE pekee haziwapi haki ya kuingia nyumbani kwako.
- Waombe maafisa wa ICE wakuonyeshe nakala ya hati ya idhini kupitia dirisha au waipitishe chini ya mlango. Hakikisha kuwa ina jina na sahihi ya hakimu.
- Ukifungulia mlango maafisa wa ICE, unawaruhusu kuingia nyumbani kwako na huenda usiweze kupinga kukamatwa kwako na maafisa wa ICE mahakamani baadaye.
- Maafisa wa ICE wanaweza kutoa taarifa za kupotosha ili kuwakamata watu walio nyumbani. Ni jambo la kawaida kwa maafisa wa ICE kusema kuwa wanachunguza kosa la uhalifu au ulaghai ili kukushawishi ufungue mlango na kuzungumza nao.
- Maafisa wa ICE wanaweza kuvalia fulana iliyoandikwa "Police" na wanaweza wasikwambie kuwa wao ni maafisa wa ICE.

**UKIKAMATWA NA POLISI**

- Ikiwa umekamatwa na kushtakiwa kwa kosa la uhalifu, sema mara moja: "Ningependa kusalia kimya" na "Ningependa kuzungumza na wakili." Ikiwa huwezi kumudu gharama za wakili, una haki ya kupata mmoja bila malipo.
- Usizungumze, usitie sahihi kwenye hati yoyote au kufanya maamuzi yoyote bila uwepo wa wakili.
- Una haki ya kupiga simu. Polisi hawawezi kusikiliza unapokuwa unazungumza kwa simu na wakili.
- Jiandae endapo utakamatwa. Kumbuka nambari za simu za wanafamilia na wakili wako. Unda mipango ya dharura ikiwa una watoto au unatumia dawa.
- Baada ya kukamatwa na polisi, taarifa za kukutambulisha, zikiwemo alama za vidole, zinaweza kushirikiwa na ICE kiotomatiki. ICE inaweza pia kupata maelezo ya nambari yako ya simu na anwani.

<u>IKIWA WEWE SI RAIA ULIYEKAMATWA NA POLISI</u>

- Ikiwa unashtakiwa kwa kosa la uhalifu, mweleze wakili wako wa uhalifu kuhusu hali yako ya uhamiaji. Madhara ya uhamiaji yanayotokana na hatia ya uhalifu yanaweza kuwa mabaya zaidi kuliko adhabu ya kosa la uhalifu lenyewe.
- Usizungumze kuhusu hali yako ya uhamiaji na mtu yeyote isipokuwa wakili wako.
- Ukiwa gerezani, afisa wa uhamiaji anaweza kukutembelea. Usijibu maswali au kutia sahihi kwenye hati yotote kabla ya kuzungumza na wakili.

- Una haki ya kukataa kutia sahihi kwenye hati zozote bila kushauriana na wakili.

**UKIWEKWA KIZUIZINI NA MAAFISA WA UHAMIAJI (“ICE”)**

- Una haki ya kuwa na wakili, lakini serikali haina wajibu wa kukupa mmoja.
- Una haki ya kuwasiliana na ubalozi mdogo wa nchi yako au kumwomba afisa ajulishe ubalozi mdogo wa nchi yako kuwa umekamatwa.
- Usizungumze kuhusu hali yako ya uhamiaji na mtu yeyote isipokuwa wakili wako. Usitie sahihi kwenye hati yoyote bila kuzungumza na wakili wako.
- Tafuta nambari yako ya A kwenye hati zako za ICE na uwape familia yako. Unahitaji Nambari hii ya A ili kupata maelezo ya mahakama ya uhamiaji na eneo unalozuiliwa.
- Una haki ya kusoma hati ambazo ICE inakupa katika lugha unayoelewa au umwombe mtu akutafsirie. Pata nakala ya hati zote ambazo ICE inakuomba utie sahihi na uzihifadhi kwenye eneo unalozuiliwa.

**UKIWASILIANA NA AFISA WA FBI**

- Ikiwa afisa wa FBI atakuja nyumbani kwako au kazini kwako, huhitajiki kujibu maswali yoyote. Mwambie afisa huyo kuwa ungependa kuzungumza na wakili kwanza.
- Ikiwa utaombwa kukutana na maafisa wa FBI kwa ajili ya mahojiano, una haki ya kusema kuwa hutaki kuhojiwa.
- Ikiwa utakubali kuhojiwa, hakikisha kuwa wakili yupo. Huhitajiki kujibu maswali yoyote ambayo hujihisi vizuri kujibu na unaweza kusema kuwa utajibu tu maswali kuhusu mada maalum.

**FARAGHA NA TEKNOLOJIA YAKO**

- Hakikisha kuwa wasifu wako wa mitandao ya kijamii ni wa faragha na ufikirie kuhusu taarifa unazoshiriki kuhusu maisha yako kwenye mitandao ya kijamii.
- Kumbuka kuwa simu yako inaweza pia kufuatilia eneo halisi ulipo wakati wowote na makampuni hushiriki taarifa hii kati yao na ICE.
- ICE itahifadhi simu yako ikiwa utakamatwa ukiwa nayo na maafisa wa ICE wanaweza kuichunguza simu yako bila ruhusa yako katika hali fulani.

**UKIHISI KUWA HAKI ZAKO ZIMEKIUKWA**

- Kumbuka: makosa ya polisi hayawezi kupingwa mtaani. Usiwazuie maafisa kukukamata kwa kupigana au kutishia kuwasilisha malalamiko.
- Andika maelezo yote unayokumbuka, ikiwemo nambari za beji za maafisa na nambari za gari la doria, shirika ambalo maafisa hao wanatoka na maelezo mengine yoyote. Pata maelezo ya mawasiliano ya mashahidi wowote. Ikiwa umejeruhiwa, piga picha za majeraha yako (lakini tafuta huduma za matibabu kwanza).
- Wasilisha malalamiko yaliyoandikwa na kitengo cha mambo cha shirika au bodi ya malalamiko ya kiraia. Mara nyingi, unaweza kuwasilisha malalamiko bila ya utambulisho wako kujulikana ikiwa ungependa iwe hivyo.
- Wasilisha malalamiko yaliyoandikwa kwa ACLU ya RI kwa kutuma barua pepe kwa info@riaclu.org, au piga simu kwa (401) 831-7171.

Kanuni tofauti zinatumika kwenye mipaka ya kimataifa na viwanja vya ndege. Kwa watu binafsi walio na viza fulani ambazo si za wahamiaji, mnaweza kuhitajika kujibu maswali kuhusu hali ya uhamiaji.

Tunategemea polisi watulinde na kututendea haki sote, bila kujali mbari, kabila, asili ya kitaifa au dini. Kadi hii inatoa vidokezo vya jinsi ya kuwasiliana na polisi na kuelewa haki zako.

**Kumbuka:** Baadhi ya sheria za jimbo zinaweza kutofautiana. Kanuni tofauti zinatumika katika vituo vya ukaguzi na wakati unapoingia Marekani (ikiwemo katika viwanja vya ndege). Brosha hii haikusudiwi kutumika kama ushauri wa kisheria.

ILISASISHWA FEBRUARI 2025

ACLU
AMERICAN CIVIL LIBERTIES UNION FOUNDATION
Rhode Island

ACLU of Rhode Island
128 Dorrance St. Ste 400
Providence, RI 02903
www.riaclu.org
(401) 831-7171